JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MI<UU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

APRIL, 2026

Dodoma

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFİSİ YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI

NAMBA ZA SIMU:

Mkuu wa Shuıe: 0752 282 394
Makamu wa Shuıe: 0764 988 373
Malezi: 0713 996 936/0764 983 747

Shule ya Sekondari Manyunyu, S.L.P. 619,
NJOVBE
..........................

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi..........
___________________________________

S.L.P...........................................
___________________________________

Yalı: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MANYUNYU ı-1ALThSHAUR1 YA WILAYA YA NJOMBE WA NJOMBE MWAKA 2026

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya____________.
Shule ya Sekondari Manyunyu ipo umbali wa Kilometa 54 Mashariki mwa Mji wa Njombe. Usafiri wa basi kutoka mjini Njombe unapatikana katika kituo cha mabasi Njombe Stendi Kuu au Kibena Madukani. Nauli ni Shilingi 8,000/— kwa basi.
Muhula wa Masomo unaanza ____________________ tarehehivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti ____________________ shuleni tareheMwisho wa kuripoti ni ______________________. tarehe Mwanao anatakiwa kuja na nakala(COPY) ya Cheti cha Kuzaliwa pamoja na nakala(COPY) ya Hati ya Matokeo (Result Slip) ya kidato cha nne. Au nakala (copy) ya cheti cha kitaaluma kidato cha nne.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:2.1 Sare za Shule
i. Sare ya shule hii ni Mashati mawili meupe Mikono mirefu na Sketi mbili ndefu (30cm kutoka kwenye goti chini) rangi ya chungwa (Carrot) na tai mbili ndefu rangi ya chungwa (Carrot) kwa Wasichana (Mshono wa Sketi ni Rinda Box ya

kunyooka (siyo "V") mbele na nyuma (kulia na kushoto ziwe rinda ndogo mbili mbili), na anaweza kushona shuleni kama imeshindikana huko); ii. Rangi ya Hijab au kijuba (Kwa Waislam) ni nyeupe isiyo na urembo wowote. Ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama kwa ajili ya kuvaa darasani na mtandio mdogo mweupe kwa ajili ya kuvaa kwenye kazi za nje.

iii. Sare ya Michezo ni sketi fupi mshono wa solo yenye urefu usawa wa goti na bukta rangi ya damu ya mzee (siyo jezi) (Zinaweza kushonwa shuleni kama itashindikana huko). Raba za michezo ni rangi nyeusi za kufunga na kamba. Tshirt rangi ya blue, shingo duara; Isiwe na maandishi wala alama yoyote.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksijozi mbili na zaidi nyeupe za shule; vi. Sweta Zito rangi ya blue la uzi, lisilo na alama yoyote. Mshono ni shingo ya V; vii. Nguo za kushindia (shamba dress). Mshono ni solo, kitambaa draft ndogondogo rangi nyeupe na nyekundu. (Linaweza kushonwa shuleni kama itashindikana huko); viii. Tracksuit rangi ya kijivu yenye mistari myeupe pembeni isiyo na kofia wala maandishi/picha.

ix. Sweta lenye shingo ndefu (Pullneck) rangi nyeusi au kijivu.

x. Tisheti (T-shirt) rangi ya kijivu yenye nembo ya shule. Itapatikana shuleni; xi. Kotijeusi lisilo na alama yoyote wala kofia lenye urefu unaolingana na urefu wa sweta la shule.

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari kuanzia 12 (Counter 3 Quire) na kalamu za kutosha; ii. Ream (A4 aina ya a one multi purpose quality paper) Mbili (2) za Karatasi kwa mwaka; iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa); iv. Aje na picha za passport 02 za hivi karibuni.

v. Dissecting Kit na Laboratory Coat kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

vi. Scientific Calculator (Kwa wanafunzi wa PCB na wote wanaosoma Geography); vii. Godoro la futi 2 $^{1}/2$ unene inchi 6.

viii. Mashuka Jozi 2 rangi nyeupe yasiyo na maua, blanket 1 zito, mto na foronya 1 rangi nyeupe, ix. Nguo za ndani za kutosha;

x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe); (visiwe vya plastiki) xi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko; (rangi ya pinki na nyeupe) xii. Aje na kadi ya BIMA YA AFYA (NHIF) kama anayo; kama hana aje na Tsh 50400/=(elfu Hamsini na mia nne ) kwa ajili ya bima ya afya.(lazima)

xiii. Aje na rula na mkebe wenye vifaa vyote; xiv. Aje na mswaki, dawa ya mswaki na sabuni za kutosha; xv. Aje na tochi, Mwamvuli, Taulo, Toilet Paper (TP), Taulo za kike (Pads); xvi, Aje na kanga za kuogea doti mbili. Siyo kikoi (haruhusiwi kuja na kikoi shuleni) xvii. Aje na begi la kubebea madaftari na tranka kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake;

Vifaa vya usafi:

ü PCB waje na mkasi Olwa kukatia maua .

ü HGL waje najembe Ol lenye mpini na siesha Ol ü HKL waje na mifagio ya ndani (soft broom 02) na siesha Ol ü HGK waje na mifagio ya chooni (hard broom 02) na mopa Ol ü HGLi waje na mifagio ya chooni (hard broom 02) na mopa Ol ü HGFa waje najembe lenye mpini (Ol) na siesha Ol

2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/- |
| 3. | Tahadhari | 5,000/- |
| 4. | Nembo | 5,000/- |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/- |
| | Jumla | 80,000/- |

Michango hii ilipwe kupitia akauntİ Nag 60606600124, NMB. Jina la Akaunti Manyunyu Secondary
School. (Fedha ya bima isilipwe kwenye akaunti)

3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Nas 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa lava Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais — TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine najamii kwa ujumla ni jambo la lazima; ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule; iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Night Preparation); iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v.Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii; Vi.Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule; vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa; viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; ix. Kutunza mali za shule;

X. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

Xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUI-IIMU:

Ü Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi; Akija nayo atarudi kuirudisha kabla ya kupokelewa ü Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kWenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu; ü Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na: i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa./utoro; iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo; iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule; Vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni; vii. Kufuga ndevu; viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya; ix. Uvutaji wa sigara;

x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa; Xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba; xii. Kusababisha mimba; xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi; xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv.Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa; xvii. Kufanyajaribio 1010te la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali; ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa yajinai; iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

NB: Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

FOMU YA

A. AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI / MLEZI 1: MWANAFUNZI

1. ____________________ ..........................

Mimikidato cha

2. Nakubali kujiunga na shule hii ya Sekondari Manyunyu nikiwa mwanafunzi wa Bweni.
3. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote, sheria na taratibu zote za shule. Nimekubali kuingia kidato cha tano katika shule ya Sekondari Manyunyu.
4. Kwa hiyo naahidi kwamba:-
   (a) Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu.
   (b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vile ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa Chama Tawala na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
   (c) Nitatunza Mali ya Umma ambayo ni pamoja na mazingira, samani (fumiture), vitabu n.k.
   (d) Sitashiriki katika mgomo wowote wala kuchochea mgomo kwa wanafunzi wenzangu.
   (e) Nitasoma kwa bidii najuhudi ili nifaulu mitihani yangu.
   (f) Nitashiriki katika shughuli nyingine mbali na masomo ya darasani.

Saini ya mwanafunzi.......................................tarehe...........................

11: MZAZI/ MLEZI

Mimi ____________________ Ninakubali mtoto wangu

Kidato cha mwaka 20...........

............................................................. Kidato cha ...............................

Tareheakiwa mwanafunzi wa Bweni/ Hostel

........................................

Kwa hiyo naahidi:-

1. Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule walimu na wafanyakazi wengine katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sheria na taratibu zote za shule na kuyatimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu
2. Nitafanya kila niwezalo ili kumwezesha mwanangu kufika shuleni mapema, kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufaulu kwa muda wote awapo shuleni.

FOMU YA

3. Anwani yangu ya kudumu ni...................................................

_______________________________________________

Saini ya mzazi / mlezi ______________________ tarehe.............................

Bill. KUWATEMBELEA WANAFUNZI / SII<U YA WAGENI

Wazazi / walezi wataruhusiwa kuwatembelea wanafunzi mara moja kwa mwezi ambayo ni kila Jumapili ya kwanza ya mwezi kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:30 jioni. Mwalimu wa zamu atakuwepo shuleni kwa muda huo kupokea wageni; hairuhusiwi kumletea mwanafunzi chakula.

## B. KUPIMA AFYA MWANAFUNZI

MANYUNYU SECONDARY SCHOOL, .

P. O. BOX 619, NJOMBE THE MEDICAL OFFICER:

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Kindly please examine ______________________________ to determine her physical and mental fitness for pursuing secondary school studies.

FOMU YA

1. Eyesight
2. Hearing........................................................................................
3. Spleen........................................................................................
4. Limbs........................................................................................
5. Epilepsy........................................................................................
6. Cardiac disease..............................................................................
7. Venereal diseases...........................................................................
8. Rheumatism.....................................................................................
9. Pregnancy.......................................................................................
10. Any other serious diseases ..........................................................
11. General comments ......................................................................

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................

MKUU WA SHULE
MANYUNYU SEKONDARI
S.L.P.619
NJOMBE

ADVERA . BAGOKA
MI<UU WA SHULE

SIGNATURE...................................................
STAMP.........................................................

D. KUANDIKISI-IWA SHULENI MWANAFUNZI

1.Jina katnili

..........................................................................................

2. Mahali ulipozaliwa ......................................................................................... 3.

Tarehe ya kuznliwa.........................................................................................

4. Uraia

..........................................................................................................

5.Anwani ya nyumbani..........................................................................................

6.Anwani ya mzazi / mlezi (kama tofnuti na hiyo hapo juu)

---

7.Jina la mzazi / mlezi

...........................................................................................

FOMU YA

Ndugu wanne (04) watakaoruhusiwa kuja kutnwona mwanafunzi akiwa shuleni.

| Picha | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Jina | | | | |
| Uhusiano | | | | |
| Namba ya Simu | | | | |

8. Dini ……………………………………………………………………………
9. Kidato unachopokelewa …………………………………………..
10. Shule unayotoka …………………………………………………………..
11. Shughuli unayopendelea mbali na masomo ya darasani kama vile mpira wa pete, riadha, kuimba n.k. ……………………………………………………………… 12. Wilaya unayotoka ………………………………… Mtaa …………………………… Kata……………………..

N.B.: Hutaruhusiwa kubadili dini, dhehebu bila uthibitisho wa barua kutoka kwa mzazi au mlezi. Barua ipitishwe na mtendaji kata unakotoka.

13. Saini ya:

Mwanafunzi……………………………………..tarehe ………………………………………………

Mzazi/mlezi ……………………………………… tarehe…………………………………………...

MATUMIZI YA OFISI TU:

Namba ya shule………………………………………………………………………………………

Namba ya mtihani……………………………………………………………………………………

# F. ORODHA NA BAADHI YA VITABU KWA KILA SOMO

## A. HISTORY

Understanding history for advanced level by B.NYAKUNGA

## B. KISWAHILI.

1. USHAIRI Dunia uwanja wa fujo, Nyerere na safari ya Hanaani
   Fungate ya Uhuru Mohamed S. Khatibu,
2. RIWAYA Vuta Nkuute Shafi Adam Shafi,
3. TAMTHILIYA: Kwenye Ukingo wa Thim Ibrahim Hussein, Morani Emmanuel Mbogo, Kivuli l<inaishi Said Mohamed, Nguzo Mama Penina Mhando,
4. Kamusi Kiswahili Sanifu-TUK1

## C. GEOGRAPHY

1. ADVANCED GEOGRAPHY 1 Review Questions &Answers
2. HUMAN and ECONOMIC GEOGRAPHY Advanced level written by DT. Msabila
3. ADVANCED PRACTICAL GEOGRAPHY Written by ZIST KAhå1L1
4. ADVANCED PHYSICAL GEOGRAPHY Written by DT.Msabila
5. SCIENTIFIC CALCUTATOR ni lazima kuja nayo kwa kila mwanafunzi anayesoma somo la Geography.

## D. ENGLISH

ANIMAL FARM
CHASING THE LEOPARD (mkuki na Nyota)
THE OPPORTUNIST ELITE Nyambali nyangwine

## E. PHYSICS

l. Advanced Level Physics (4th Edition ) (1993) by Muncaster 2. Principle of Physics for Class Xll (2007) By Mehta, V.K& Mehta R.
3. Advanced Physics (5th Edition). (2000) By Duncan, T.

## F. CHEMISTRY

1. Conceptual chemistry for class Xi and Xii
2. Understanding Chemistry

## G. BIOLOGY


1. Biological science third by D.J. Taylor, N.P.O Green and G.W. Stout
2. Advanced biology principle and application by CJ Clegg and DG McKean. 3. New understanding biology for advanced level by Glenn and Susan Toole
4. Plant and animal biology volume 2 by AE vines and N Rees.
5. for class XI&XII by Dr. P.S. Verma and Dr. B.P. Pandey,

H. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

J. Advanced level general studies notes form 5 & 6 by Nyambari Nyangwine

10

KARIBU SANA KATIKA SHULE 1-111

Saini ya Mkuu wa Shule: 

SHULI: SEKONDAP

Jina laMkuu wa Shule: ADVERAJ. BAGOKA

Mhuri wa NflCUU wa Shule:

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamelQ1wa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USIT1-nvŒ CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

> Mkuu wa shule: 0752 282 394
> Makamu wa Shule: 0764 988 373
> Mwandamizi Taaluma: 0759 101 976
> Mwandamizi Malezi: 0764 983 747